

OMAR BABU MARJAN “ABU MARJAN”

14 Julai 1967 – 20 Januari 2015

KUMBUKUMBU YA KUMUENZI MWENZETU MAREHEMU

HEZEKIEL GIKAMBI¹

Jamii ya wataalamu na wapenzi wa Kiswahili kwa jumla walio Afrika Mashariki na kote ulimwenguni walipata pigo kubwa mnamo tarehe 20 Januari 2015 kwa kifo cha Omar Babu almaarufu Abu Marjan katika hospitali ya Avenue jijini Nairobi baada ya kuugua saratani ya kongosho na ya ini kwa muda mfupi. Omar Babu aliwaacha mkewe Fatma Ghalib akiwa na wanawe Ashraf na Rumeida.

Kuondoka kwa Omar katika ulingo wa lugha ya Kiswahili kumeacha pengo kubwa sana kwa kuwa msomi huyu alikuwa mwandishi, mshairi wa kutajika na mkereketwa wa lugha hii aliyekuwa ameanza kutambulika na wenzake kama balozi wa Kiswahili kwa jinsi alivyojitolea kukitetea na kukiendeleza.

Kufikia kifo chake Omar Babu alikuwa mhadhiri wa lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Köln (Cologne) nchini Ujerumani ambako pia alikuwa ameanza kujiandaa kwa masomo ya udaktari katika Masomo ya Afrika. Chambilecho aliyekuwa mwanafunzi wake Dk Andrea Hollington, wanafunzi na walimu wenzake walimheshimu na kumpenda sana marehemu kwa sababu ya tabia yake ya upole na subira.

Omar alizaliwa mjini Chuka mnamo 1967 katika sehemu iliyokuwa wilaya ya Meru zamani ambayo ni Kaunti ya Tharaka Nithi sasa na kuanzia masomo yake katika Shule ya Msingi ya Chuka mnamo 1973 na kukamilisha mnamo mwaka wa 1980. Baada ya hapo Omar alijiunga na Shule ya Upili ya Chuka kutoka mwaka 1981 hadi mwaka 1984 na kuhitimishia elimu yake ya shule huko Shule ya Upili ya Mbiruri mwaka 1986 kabla hajajiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi kusomea shahada ya kwanza katika anthropolojia na kujikita katika lugha na fasihi ya Kiswahili.

Baada ya kufuzu chuoni humo Omar Babu alifanya kazi katika Makavazi ya Kitaifa Kenya kama afisa wa kutunza habari za makavazi kabla ya kujiunga na kampuni ya usambazaji habari ya Nation Media Group katika kitengo cha redio na televisheni kama mtafsiri na mwanahabari. Omar Babu amejikuta katika mabara yote ulimwenguni akisoma ili kujiendeleza katika taaluma

¹ Tunawashukuru Abdilatif Abdalla, Ahmed Hussein Ahmed Parkar, James Mwilaria, Andrea Hollington na Nico Nassenstein kwa kutusaidia kuongezea taarifa hapa na pale. *Hezekiel Gikambi pamoja na Lutz Diegner kwa niaba ya wahariri wote wa Swahili Forum.*

HEZEKIEL GIKAMBI

ya lugha, utamaduni au uanahabari. Si ajabu hamu ya kujiongezea maarifa ilimsukuma kutoka Nation Media Nairobi na kuelekea Marekani katika Chuo Kikuu cha Ohio alikosomea shahada ya umahiri ya taaluma za Kiafrika na baada ya kuhitimu na kufundisha Kiswahili chuoni humo akajikuta akielekea Ulaya katika Chuo kikuu cha Cologne nchini Ujerumani alikokuwa anafundisha Kiswahili. Alipokuwa Marekani katika Chuo Kikuu cha Ohio aliwahi kukutana na rafiki yake wa muda mrefu Ken Walibora Waliaula ambaye pia alisomea katika chuo hicho. Pia alisoma kozi ya uanahabari kwenye programu ya masomo ya mbali ya chuo kimojawapo nchini India.

Omar Babu ni mwandishi wa kazi kadha za kinathari na za kishairi kama vile riwaya za *Kala Tufaha* (2007) na *Heri Subira* (2010), na hadithi fupi nyingi kama vile ‘*Ndoa ya Samani*’ katika mkusanyiko wa *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007) na ‘*Pendo la Siri*’ katika mkusanyiko wa *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* (2007). Vilevile alitafsiri hadithi kadhaa katika mkusanyiko wa *Jua Linapotua na Hadithi Nyingine* (2011). Mwaka 2011 alihariri mkusanyiko wa hadithi fupi uitwao *Kopo la Mwisho na Hadithi Nyingine* ulio na hadithi zake tatu ‘*Baa la Njaa*’, ‘*Lofa*’, na ‘*Kopo la Mwisho!*’, pamoja na nyingine za waandishi mashuhuri kama Mohamed Suleiman Mohamed na Ngũgĩ wa Thiong’o (tafsiri ya Kitula King’ei). “*Abu Marjan*” alitunga mashairi zaidi ya mia tano yaliyochapishwa katika diwani mbalimbali, zikiwemo katika *Diwani ya Karne Mpya* (2007) na *Waja Leo* (2012) zilizohaririwa na Ken Walibora na katika *Ambari* (2012) iliyohaririwa na Ahmed Hussein. Mwaka 2014 tafsiri zake za Kiingereza za mashairi ya kumuenzi Marehemu Profesa Thomas Geider (1953-2010) yaliyotungwa na Mwalimu Hassan Adam, Mhadhiri wa Kiswahili aliyefundisha miaka mingi sana katika nafasi ya Omar Babu katika Chuo Kikuu cha Koloni kabla hajastaafu, na Kyallo Wadi Wamitila.

Licha ya hadhi hii ya kimasomo, utarazaki na pia uandishi wa kazi kadhaa, “*Abu Marjan*” ama “*Bu Ashraf*” alikuwa ni mtu aliyependa kutangamana na watu wa kila tabaka, mpole na mnyenyekevu ajabu, na alipenda sana kusikiliza maoni ya wengine. Katika umri wa miaka 47 alipofariki Omar Babu alikuwa tayari kajizolea sifa za mtaalamu wa Kiswahili wa kimataifa aliyekuwa na umilisi wa lugha hii, siyo tu katika uandishi wa bunilizi ila pia katika usemaji wake na utunzi wa mashairi.

Alipokuwa Ujerumani hadi kifo kilipomchukua, kazi na sifa zake za kishairi na kuhusu uchanganuzi wa masuala anuwai ya isimu na fasihi ya Kiswahili zilisikika na kuhisika kote ulimwenguni. Hili liliwezekana kwa kiasi fulani kupitia machapisho ya tungo zake katika gazeti la *Taifa Leo* na tovuti ya *Swahilihub* na kwa kiasi kikubwa kupitia kwa mitandao mbalimbali ya kijamii ya kielekroniki. Omar alishiriki katika mijadala mikali mikali na kutunga mashairi katika kumbi mbalimbali kama zile zilizotajwa, na kwingineko kama vile *Umoja wa Washairi*, *Nuru ya Lugha* na *Umbuji na Ulimbembwende wa Kiswahili*, miongoni mwa nyingi nyingine.

KUMBUKUMBU YA OMAR BABU MARJAN

Katika mazishi yake kwenye makaburi ya Kariokor jijini Nairobi mnamo tarehe 21 Januari 2015 kila aliyekuwepo alipata kufahamu jinsi marehemu alivyokuwa anahusiana na watu na makundi mbali mbali kupitia lugha ya Kiswahili. Walikuwepo waandishi wa vitabu vya Kiswahili, walimu, washairi, wanahabari wa Kiswahili na watu wa taaluma na matabaka mbalimbali.

Jumbe za rambirambi zilifurika katika majukwaa ya kijamii ya kidijitali, redioni na magazetini kutoka siku ya kifo chake. Majukwaa yanaendeleza lugha ya Kiswahili hasa ndiyo yaliyoshika usukani katika kueleza umma pengo lililoachwa na marehemu katika ulingo wa kukipigania Kiswahili. Wengi walihisi kuwa Omar Babu alikuwa miongoni mwa waandishi waliokuwa wanaibukia aliyekuwa na kipawa adimu katika ubunifu wa kazi za Kiswahili.

Jumuiya ya wataalamu wa Kiswahili walio katika taasisi kama vyo vya vyombo vya habari barani Ulaya, hasa Ujerumani alikuwa akitarazaki Omar, walishiriki kikamilifu katika maombolezi ya mwenzao. Wataalam wenzake na jumuiya ya wanafunzi wa elimu ya Afrika ya Chuo Kikuu cha Cologne, hasa Profesa Anne Storch, Dk Andrea Hollington, Dk des. Nico Nassenstein, na Bi Gabriela Aguirre wa chuo hicho, pamoja na Profesa Clarissa Vierke wa Chuo Kikuu cha Bayreuth, wasomi waishio Ujerumani walifuatilia msiba huo kwa karibu sana na hata kusaidia kwa michango ya hela za kusaidia familia ya marehemu na masuala mengine yaliyohitaji urasimu baina ya familia ya marehemu na mwajiri wake Chuo Kikuu cha Cologne. Mbali na Chuo Kikuu cha Cologne, Chuo Kikuu cha Bayreuth kulikuwa kama nyumbani kwake kwa kitaaluma pia hasa kwa kushiriki kwake katika makongamano ya Kiswahili ya kila mwaka. Hakuwahi kukosa kongamano hilo tangu aende Ujerumani ila alilikosa katika miaka miwili kabla ya kifo chake kwa sababu ya changamoto za kiafya.

Sifa moja mahsusi iliyodhihirika katika jumbe hizo sio tu kuhusu nafasi ya Omar Babu Marjan katika uendelezaji wa lugha ya Kiswahili ila pia kuhusu hulka yake iliyomwelezea kama mtu mkarimu, mwenye utu, mpole na mnyenyekevu, aliyetangamana na watu wa matabaka yote kwa urahisi sana na aliyekuwa tayari kusaidia kwa vyovyote hata kama ilibidi ajinyime mwenyewe.

Baadhi ya taarifa zilizoandikwa kuhusu kifo chake katika magazeti zilimuita “Amri Jeshi” wa lugha ya Kiswahili kulingana na jinsi alivyoonyesha kuwepo kwake katika mitandao ya kijamii katika uteteaji wa lugha ya Kiswahili. Makini yake katika kutambua lilipo kosa katika lugha kwenye msemu au maandishi iliwashangaza wengi. Pia alipata muda wa kuandika angalau beti mbili tatu za Kiswahili hata kama ni katika kujibu swali kuhusu Kiswahili au jambo tofauti kwa Kiswahili. Mtazamo wake wa kiusomi ni kuwa kila siku ni fursa ya kujifundisha na mtu anaweza kujifunza kutoka popote au kwa yeyote. Alipinga daima kuwa yeye ni gwiji wa Kiswahili kwa kuwa anahisi kuwa bado hakuwa ameifikia hadhi hii.

HEZEKIEL GIKAMBI

Hadi kufikia kifo chake Omar Babu “Abu Marjan” alikuwa na miswada mingi iliyosubiriwa kuchapishwa. Muswada mmojawapo ambao umefahamika na wengi ni wa diwani ya mashairi yake iitwayo *Sambo ya Umalenga* [bado haijchapishwa]. Imehaririwa na Abdilatif Abdalla, mtunzi maarufu wa *Sauti ya Dhiki* (1973), na mmoja wa washairi waliomjenga na kumwongoza Omar Babu. Kabla kuzidiwa na ugonjwa na hatimaye kufariki Omar alikuwa ameanza kujiandaa kwa masomo ya uzamivu katika Masomo ya Afrika akimakinikia tungo za kasida. Familia yake, ndugu, jamaa, marafiki na jumuiya ya wasomi watamkosa sana Omar Babu. Mungu aiweke roho yake mahali pema.

Tungo za Omar Babu Marjan “Abu Marjan”

Riwaya

2007. *Kala Tufaha*. Nairobi: Phoenix.

2010. *Heri Subira*. Nairobi: Oxford University Press.

Uhariri wa mkusanyiko wa hadithi fupi

2011 (mh.). *Kopo la Mwisho na Hadithi Nyingine*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Hadithi fupi

2007. ‘*Ndoa ya Samani*’. Said Ahmed Mohamed & Ken Walibora (wah.). *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. k. 98-105.

2007. ‘*Pendo la Siri*’. Peter I. Iribemwangi (mh.). *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*. k. 119-131.

2011. ‘*Baa la Njaa*’. Omar Babu (mh.). *Kopo la Mwisho*. k. 1-11.

2011. ‘*Lofa*’. Omar Babu (mh.). *Kopo la Mwisho*. k. 98-109.

2011. ‘*Kopo la Mwisho!*’. Omar Babu (mh.) *Kopo la Mwisho*. k. 135-144.

2012. ‘*Hajiri Ahajiri!*’. Ken Walibora (mh.). *Maskini Milionea na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Oxford University Press. k. 92-103.

2011. ‘*Masaibu ya Huba*’. Clara Momanyi & Rayya Timammy (wah.). 2012 [toleo jipya]. *Takrima Nono na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Longman Kenya. k. 143-153.

2011. ‘*Hemedi Ajuta !!!*’. Ken Walibora & Peter I. Iribemwangi (wah.). 2012 [toleo jipya]. *Sina Zaidi na Hadithi Nyingine*. k. 52-68.

KUMBUKUMBU YA OMAR BABU MARJAN

2015. 'Kwambizana Kweli.' Said Ahmed Mohamed & Ken Walibora (wah.). *Homa ya Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Phoenix. k. 53-62.

Tafsiri za Kiingereza-Kiswahili

2011. Miriam Osore (mh.). *Jua Linapotua na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Longhorn. (Tafsiri ya Emelia Ilieva & Waveney Olembo (wah.). 2010. *When The Sun Goes Down and Other Stories from Africa and Beyond*. Nairobi: Longhorn/Sasa Sema.)

'Safari ya Ughaibuni'. Tafsiri ya 'Twilight Trek' ya Sefi Atta, mwandishi wa Nigeria.

'Kwenda Masomoni Ng'ambo'. Tafsiri ya 'Leaving' ya Moyez G. Vassanji.

Mashairi

Omar Babu ametunga mashairi zaidi ya mia tano. Yafuatayo ndiyo yale ambayo tumeweza kukusanya taarifa zake za uhakika kuwa yamechapishwa ama kuhaririwa.

2007. Ken Walibora (mh.). *Diwani ya Karne Mpya*. Nairobi: Phoenix.

'Ajali Ikidhiringi'. uk. 49.

'Kiumbe Kujishauwa'. uk. 51.

'Ndizi Gani?'. uk. 95.

'Ugomvi wa Ndizi'. uk. 111.

'Kusemezana ni Kupatana'. uk. 44.

'Msitu ni Ule Ule'. uk. 29.

'Sisi Ikiwa si Mimi'. uk. 32.

'Kwenda Mbio sio Kupata'. uk. 58.

'Rangi ya Paka si Hoja'. uk. 103.

2012. Ahmed Hussein (mh.). *Ambari. Diwani ya Kipekee ya Mashairi*. Mashairi ya Alamin Siwa Somo (Malenga wa Mombasa), Mohammed Shabaan Ali (Mpembuzi Mchanga), Omar Babu (Abu Marjan) na Khamis Darwesh (Mpwamu). Mombasa: Chesil Printers.

'Alhamdulillah!'. uk. 1.

'Hakuna Bingwa wa Bingwa!', uk. 3.

'Jitu Limetukoma!'. uk. 4.

'Kattu Sitezi Foriti!'. uk. 5.

HEZEKIEL GIKAMBI

- ‘Zidi Kulipiga Domo!’ . uk. 11.
‘Ewe Nyonda!’ . uk. 15.
‘Ninakupenda Habibu!’ . uk. 26.
‘Kichungu Ama Kitamu!’ . uk. 37.
‘Kulla Avaao Suti!’ . uk. 40.
‘Mtu Hangilii Kondo!’ . uk. 46.
‘Sione Kufika Sasa!’ . uk. 51.
‘Tungajitapa Wajuzi’ . uk. 54.
‘Usione Utajiri!’ . uk. 61.
‘Wamkanusha Rahimu!’ . uk. 62.
‘Waswahili ni Wajuzi!’ . k. 65-66.
‘Bahari Imechafuka!’ . uk. 69.
‘Hiyau Mawi Yawile!’ . uk. 71.
‘Mpawa Hapokonyeki!’ , uk. 80.
‘Nalia na Langu Jito’ . uk. 82.
‘Sikhadawe ni Pelezi!’ . uk. 87.
‘Sitokimbiza Upepo!’ . uk. 88.
‘Viwi Kuviramba Vyombo!’ . uk. 89.
‘Nasubiri!’ uk. 99.

2012. Ken Walibora (mh.). *Waja Leo*. Nairobi: Oxford University Press.

- ‘Moyo Wangu!’ . uk. 6.
‘Wapishi Leo!’ . k. 18-19.
‘Kupe!’ . uk. 28.
‘Zama za Wavyele!’ . k. 34-35.
‘Sikutaki!’ . uk. 43.
‘Waja Leo’ . uk. 71.

KUMBUKUMBU YA OMAR BABU MARJAN

[diwani bado haijatoka]. Omar Babu. *Sambo ya Umalenga*. Diwani yenye mashairi sabini na nne iliyohaririwa na Abdilatif Abdalla.

Tafsiri za Kiswahili-Kiingereza

2014. Hannelore Vögele, Uta Reuster-Jahn, Raimund Kastenholz & Lutz Diegner (wah.). *From the Tana River to Lake Chad: Research in African Oratures and Literatures. In memoriam Thomas Geider (Mainzer Beiträge zu Afrikaforschung 36)*. Köln: Köppe.

‘Thomas Geider.’ Tafsiri ya shairi la Kiswahili la ‘Thomas Geider’ la kumuenzi Marehemu Profesa Thomas Geider lililotungwa na Hassan Adam. uk. 222.

‘I Remember You... Thomas Geider.’ Tafsiri ya shairi la Kiswahili ‘Nakukumbuka... Thomas Geider’ la kumuenzi Marehemu Profesa Thomas Geider lililotungwa na Kyallo Wadi Wamitila. k. 224-227.